KAULI YA TAARIFA YA CHANJO

# Chanjo ya DTaP (Dondakoo, Pepopunda, Kifaduro): *Unachohitaji Kujua*

Many Vaccine Information Statements are available in Swahili and other languages. See www.immunize.org/vis

Kauli nyingi za taarifa ya chanjo zinapatikana katika Kiswahili na lugha nyinginezo. Angalia www.immunize.org/vis

## 1. Kwanini unahitaji kuchanjwa?

**Chanjo ya DTaP** inaweza kuzuia **dondakoo**, **pepopunda**, na **kifaduro**.

Dondakoo na kifaduro husambaa kutoka kwa mtu mmoja hadi kwa mwingine. Pepopunda huingia mwilini kupitia sehemu zilizokatwa au vidonda.

- **DONDAKOO (DIPHTHERIA – D)** inaweza kupelekea matatizo ya kupumua, moyo kushindwa kufanya kazi, kulemaa, au kifo.
- **PEPOPUNDA (TETANUS – T)** husababisha misuli kuwa migumu na maumivu. Pepopunda inaweza kupelekea matatizo mabaya ya kiafya, ikijumuisha kutoweza kufungua mdomo, kuwa na matatizo ya kumeza na kupumua, au kifo.
- **KIFADURO (PERTUSSIS –aP)**, unaojulikana pia kama "whooping cough," unaweza kusababisha kukohoa kusikodhibitika, kubaya sana kwamba inakuwa vigumu kupumua, kula, au kunywa. Kifaduro kinaweza kuwa kibaya sana hasa katika watoto wachanga na watoto, kikisababisha nimonia, mipapatiko, kuharibika kwa ubongo, au kifo. Katika vijana na watu wazima, kinaweza kusababisha kupoteza uzito, kushindwa kudhibiti mkojo, kuzirai, na kuvunjika kwa mbavu kutokana na kukohoa vibaya.

## 2. Chanjo ya DTaP

DTaP ni kwa watoto wachanga chini ya miaka 7. Chanjo tofauti dhidi ya pepopunda, dondakoo, na kifaduro (Tdap na Td) zinapatikana kwa ajili ya watoto wa umri zaidi, vijana, na watu wazima.

Inapendekezwa kwamba watoto wapokee dozi 5 za DTaP, kwa kawaida katika umri ufuatao:

- miezi 2
- miezi 4
- miezi 6
- miezi 15–18
- miaka 4–6

DTaP inaweza kupeanwa kama chanjo kivyake, au kama sehemu ya chanjo ya mchanganyiko (aina ya chanjo ambayo huunganisha zaidi ya chanjo moja pamoja kwa sindano moja).

DTaP inaweza kupeanwa wakati mmoja na chanjo zingine.

## 3. Zungumza na mtoa huduma za afya wako

Mwambie mtoa huduma ya chanjo wako ikiwa mtu anayepokea chanjo:

- Amekuwa na **mmenyuko wa mzio baada ya dozi ya awali ya chanjo yoyote ambayo inakinga dhidi ya pepopunda, dondakoo, au kifaduro**, au ako na **mmenyuko wowote mbaya sana wa mzio, wa kutishia maisha**
- Amekuwa **mahututi, kupungua kwa hali ya kuwa na fahamu, au mipapatiko ya muda mrefu ndani ya siku 7 baada ya dozi ya hapo awali ya chanjo yoyote ya kifaduro (DTP au DTaP)**
- Ako na **mipapatiko au tatizo lingine la mfumo wa neva**
- Amewahi kupatwa na Ugonjwa wa **Guillain-Barré Syndrome** (pia unaoitwa "GBS")
- Amekuwa na **maumivu makali au kufura baada ya dozi ya hapo awali ya chanjo yoyote ambayo inakinga dhidi ya pepopunda au dondakoo**

Katika baadhi ya visa, mtoa huduma za afya wa mtoto wako anaweza kuamua kuahirisha chanjo ya DTaP hadi katika ziara ya baadaye.

U.S. Department of Health and Human Services
Centers for Disease Control and Prevention

Watoto walio na magonjwa madogo madogo, kama vile mafua, wanaweza kuchanjwa. Watoto ambao ni wagonjwa kwa wastani au wagonjwa vibaya wanapaswa kwa kawaida kungojea hadi wapone kabla ya kupokea chanjo ya DTaP.

Mtoa huduma za afya wa mtoto wako anaweza kukupatia habari zaidi.

## 4. Hatari za mzio dhidi ya chanjo

- Maumivu au kufura kwenye eneo la sindano, joto jingi, kuudhika haraka, kuhisi mchovu, kupoteza hamu ya kula, na kutapika wakati mwingine hutokea baada ya chanjo ya DTaP.
- Athari mbaya zaidi za mzio, kama vile mipapatiko, kulia bila kikomo kwa saa 3 au zaidi, au joto jingi (zaidi ya 40.5°C [105°F]) baada ya chanjo ya DTaP hutokea mara chache zaidi. Ni nadra, kuchanja kufuatwe na kufura kwa mkono mzima au mguu, haswa kwa watoto wa umri mkubwa zaidi wakati wanapopokea dozi yao ya nne au tano.

Kama ilivyo na dawa yoyote ile, kuna uwezekano nadra sana kwa chanjo kusababisha mmenyuko mbaya wa mzio, majeraha mengine mabaya, au kifo.

## 5. Na je, kukiwa na tatizo hatari?

Mmenyuko wa mzio unaweza kutokea baada ya mtu aliyechanjwa kuondoka kliniki. Ikiwa utaona ishara za mmenyuko mbaya wa mzio (mabaka, kuvimba uso na koo, matatizo ya kupumua, moyo kudunda kwa kasi, kizunguzungu, au udhaifu), pigia simu **9-1-1** ili mtu huyo apelekwe kwenye hospitali iliyo karibu.

Kuhusu ishara zingine ambazo zinakupatia wasiwasi, pigia simu mtoa huduma za afya wako.

Mizio hatari inapaswa kuripotiwa kwa Mfumo wa Kuripoti Matukio Mabaya ya Chanjo (Vaccine Adverse Event Reporting System - VAERS). Mtoa huduma za afya wako kwa kawaida ataweka faili ya ripoti hii, au unaweza kufanya hivyo mwenyewe. Tembelea tovuti ya VAERS katika [www.vaers.hhs.gov](www.vaers.hhs.gov) au piga simu **1-800-822-7967**. *VAERS ni ya kuripoti mizio pekee, na wafanyikazi wa VAERS hawapeani ushauri wa kimatibabu.*

## 6. Mpango wa Kitaifa wa Ufidiaji wa Majeraha ya Chanjo

Mpango wa Kitaifa wa Ufidiaji wa Majeraha ya Chanjo (National Vaccine Injury Compensation Program - VICP) ni mpango wa serikali kuu ambao ulibuniwa ili kufidia watu ambao huenda walijeruhiwa na baadhi ya chanjo. Madai kuhusiana na majeraha au vifo vinavyodaiwa kutokana na kuchanjwa yako na kikomo cha muda kwa kufaili, ambao unaweza kuwa mchache kama vile miaka miwili. Tembelea tovuti ya VICP katika [www.hrsa.gov/vaccinecompensation](www.hrsa.gov/vaccinecompensation) au piga simu **1-800-338-2382** ili kujifunza kuhusu mpango huu na kufaili dai.

## 7. Je, ninawezaje kujifunza mengi zaidi?

- Muulize mtoa huduma za afya wako.
- Pigia simu idara ya afya eneo lako au ya jimbo.
- Tembelea tovuti ya Utoaji wa Chakula na Dawa (Food and Drug Administration - FDA) upate machapisho ya vifurishi vya chanjo na taarifa ya ziada katika [www.fda.gov/vaccines-blood-biologics/vaccines](www.fda.gov/vaccines-blood-biologics/vaccines).
- Wasiliana na Vituo vya Udhibiti na Uzuiaji wa Magonjwa (Centers for Disease Control and Prevention - CDC):
  - Pigia simu **1-800-232-4636** (**1-800-CDC-INFO**) au
  - Tembelea tovuti ya CDC katika [www.cdc.gov/vaccines](www.cdc.gov/vaccines).

Swahili translation provided by Immunize.org